Injili Inatosha

na

Ellis Forsman

Injili Inatosha

na

Ellis Forsman

Januari 14, 2012

Injili Inatosha

Warumi 1:16

Waru. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili ya Kristo: kwa maana ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye; kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*"

Hapa, Mtume Paulo anaweka wazi kwamba injili ya Kristo ni "*uweza wa Mungu uuletao wokovu*" – kwamba ni "*Uweza*", na uwezo wa kutosha kuweza kuokoa nafsi ya mwanadamu.

Injili ya Kristo, sheria ya Mungu inayotolewa kwa wenye dhambi na sheria yake ya muongozo kwa Wakristo, imefunuliwa kupitia Roho Mtakatifu, na ikarekodiwa katika Agano la Kale, ni muongozo pekee ambao mwanadamu anahitaji kuweza kufanikisha kuachiwa kwake kutoka dhambini, na kufurahia wokovu wa milele mbinguni.

Ufunuo wa yongeza zote au mafundisho, desturi zote na makataa yote lazima zichukuliwe kama vitu vya ziada, hayana kazi, vinaangamiza, na hivyo zinapaswa kukataliwa.

Kulikuwa na watu wakati wa siku za Paulo waliojaribu kufundisha "*injili nyingine*", na aliwaonya ndugu wa Galatia kuhusu mafundisho kama hayo ya uongo.

Wagal. 1:6-9, "*Nastajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine ; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaniwe.*"

Hebu na tuangalie baadhi za njia ambazo injili inatambuliwa katika maandiko ambayo inatumika kama ukweli usiyopingika kwa kutosha kwake kote.

Injili imekamilika

Yakob. 1:25, "*Lakini aliyeitazama sheria kamili iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*

Hiyo iliyokamili haiwezi kuendelezwa kwa kuongeza au kuondoa.

Zaidi sana, hiyo iliyo kamili haiwezi kuwa na kitu chochote kilichoongezwa au kuondolewa kutoka kwake bila kuoanisha ukamilifu wake.

Ufu. 22:18-19, "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Sheria ya Musa isingeweza kuleta ukamilifu.

Waeb. 7:19, "*Kwa maana ile sheria haikukamilisha neno; na pamoja na hayo kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri zaidi, ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu.*"

Kwa hiyo, sheria ya Musa ilikuwa tu "*kivuli cha mambo mazuri yaliyotarajiwa.*"

Waeb. 10:1, "*Basi torati kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwa kamilisha wakaribiao.*"

Sheria ya Musa haikuwa kamilifu na ilikuwa ichanwe kabla ya sheria iliyobora kuwekwa mahali pake.

- Waeb. 9:8, "*Roho Mtakatifu akionyesha neno hili, ya kwamba njia ya kupaingia patakatifu ilikuwa haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimama.*"
- Waeb. 10:4, "*Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*"
- Waeb. 10:9, "*Ndipo aliposema tazama nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili.*"

Injili ina nguvu

Waru. 1:16, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Neno "*Uweza"* katika kifungu hiki ni neno la Kiyunani "dunamis".

Hili ni neno tunalopata maneno kama “enye nguvu”, “dynamo”, na “enye nguvu kali”.

Kwa hiyo, injili inanguvu; ni dynamo ya Mungu, au “ina nguvu sana” katika wokovu. Ni mpango pekee ambao Mungu nguvu yake katika wokovu wa mwanadamu.

Huu ni mpango wa Mungu; si kitu cha mwanadamu.

Si hadithi na mpango usiyosaidia, bali ni “kubwa sana”

2 Wakor. 10:4, “*(Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;)*”

Lazima ikumbukwe kwamba injili ya Kristo ni uweza wa Mungu “*katika wokovu”;* hiyo ni katika kukombolewa kutoka dhambini na kifo na matokeo ni wokovu mbinguni.

Hivyo, kama nikitamani kuokoa nafsi, nina paswa kuhubiri injili ile ile ambayo Paulo alihubiri, kwa sababu kifupi chake hakuna uwezo ambao utawaokoa wanadamu kutoka dhambini.

Kama nikipendezwa na eneo la kijamii, na nikatoka nje na kuwasaidia watu waendelee katika maisha haya ya kimwili, lazima niyafanye vyema.

Lakini, kama niko kwa ajili ya wakovu wa nafsi, kama ninajaribu kuwapa wanadamu si tu maisha mazuri hapa, bali pia taraja la uzima wa milele baada ya hapa, basi napaswa kuwapelekea kile kinachoweza kufikia mioyo yao na kuwaokoa kutoka dhambini.

Na hiyo ndiyo injili ya Kristo.

Yesu alifuatwa na mtu aliyekuwa anawajibika na mambo ya kipekee ya kijamii.

Luka 9:57-60, “*Nao walipokuwa wakienda njiani, mtu mmoja alimwambia, nitakufuata kokote utakakokwenda. Yesu akamwambia, Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana pa kujilaza kichwa chake. Akamwambia mwingine, Nifuate. Akasema Bwana nipe ruhusa kwanza nika mzike baba yangu. Akamwambia waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu.*”

Ni jukumu lipi ambalo Yesu aliona ni muhimu?

Injili imekamilika

2 Tim. 3:16-17, “*Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*”

Injili inayotosha na kwa hakika inafaa na inatolewa katika Biblia ili kuweza kukidhi mahitaji ya familia za binadamu inasisitizwa katika kifungu hiki. Wakristo wanaamini hili.

2 Petr. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wake na Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*"

Kwa karne nyingi Wakristo wamekuwa wakionywa kuzungumza kama Biblia inavyozungumza.

1 Petr. 4:11, "*Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.*"

Kwa mimi kukubali adithi, kitabu fulani, katekisimu, kitabu cha muongozo, au kitabu cha maombi ili kitawale kazi zangu za kidini, itakuwa ni kuharibu imani yangu katika injili inayotosha ya maandiko.

Kama Biblia "*inamkamilisha mtu wa Mungu katika kila tendo jema*", sasa kwa nini kuwe na kitabu kingine ambacho si maandiko?

Si kitabu kilichotungwa na mwanadamu ambao unaukosefu wa kuaminiwa katika injili yote inayotosha ya maandiko matakatifu?

Hebu tuangalie baadhi ya mambo yaliyofundishwa katika 2 Tim. 3:16-17.

2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa katika kila tendo jema.*"

Kwamba maandiko matakatifu "*yanatolewa na pumzi ya Mungu*".

Hii inatofautisha maandishi, au maneno, ya Mungu na vitabu vilivyoandikwa na wanadamu.

Kwamba maandiko matakatifu "*lafaa*". Lafaa kwa lipi?

Lafaa kwa "*mafundisho*", au kufundisha, hiyo ni, yanaonyesha mafundisho ya Mungu na ya Kristo.

Yanafaa kwa "*kwa kuwaonya watu makosa yao*."

- Waef. 5:11, "*Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali myakemee.*"
- 2 Tim. 4:2, "*Lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumivu wote na mafundisho.*"

Yanafaa, "*Kuwaonya.*" Yana muongoza mtu katika marekebisho, au kunyoosha, maisha.

Injili ni inatosha na inanguvu njia za kurejesha maisha ya mtu.

Yanafaa "*Kwa kuwaadibisha katika haki*". Injili ya Kristo inatoa muongozo katika utakatifu na kuishi sahihi.

Kwamba maandiko matakatifu yanatolewa "*Ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa katika kila tendo jema.*"

Hiyo ni, injili inamkamilisha mtu wa Mungu katika magizo yote yanayohitajika katika maisha yake kamilifu. Hivyo, Biblia inatosha katika kila hitaji la mwanadamu la kukua kiroho.

Injili ni uvumilivu

Math. 24:35, "*Mbingu nan chi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*"

1 Petr. 1:25, "*Bali neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.*"

Vile vile, neno la Bwana haliondolewi, rekebishwa, bali liko pale pale.

Falme zinainuka na kuanguka, ufalme unakuja na kuondoka; lakini neno la Mungu linakaa.

Mfumo wa injili ni mzuri leo sawa na jinsi ilivyokuwa kwanza ilipofunuliwa kwa mwanadamu, na ina uwezo mwingi wa kuokoa sasa kama ilivyokuwa kwanza inatumika katika moyo wa mwanadamu.

Baadhi ya wanadini wanao jiingiza leo watasikiwa wakisema, "Tunahitaji injili mpya kwa kizazi kipya."

Lakini mwanadamu haitaji injili mpya kuliko anavyohitaji mwanga wa jua au chakula kipya.

Mwanadamu hajageuka kimwili hata kiakili; dhambi haija badilika. Shetani hajabadilika; hivyo, kwa nini unajaribu matakwa ili uishinde dhambi?

Kwa sababu neno litakaa milele, ni kwa ajili yake ndiyo tutahukumiwa.

Yohana 12:48, "*Yeye anikataaye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anayeamhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"

Paulo akasema katika Waru. 2:16, "*Katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawa sawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu.*"

Hitimisho

Kwa vile neno la Kristo, injili, ni kamilifu, inanguvu, imekamilika, na inavumilia, kwa nini isiwaokoe wanadamu wote?

Mungu ametuhakikishia kwamba neno lake linapohubiriwa kwamba haliwezi kurudi bila cho chote.

Isa. 55:11, "*Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa change; halitarudi bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.*"

Kama haiokoi wanadamu wote, haiokoi kwa sababu Mungu hapendi iwe hivyo.

- 1 Tim. 2:4, "*Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyokweli.*"
- 2 Petr. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyo kudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba.*"

Tatizo ni kwamba baadhi hawatakuja kwa Mungu. Yesu aliwaambia baadhi katika siku zake:

Yohana 5:40, "*Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.*"

Kama leo wewe si Mkristo, basi itii injili, "*ambao ni uweza wa Mungu wa wokovu.*"

- Mwamini Yesu kwa moyo wako wote.
- Geuka kutoka dhambini kwa ukweli na toba ya ndani.
- Kiri imani yako katika jina la Yesu
- Ubatizwe katika Kristo katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

Alafu uendelee kuishi kama injili ya Kristo inavyoongoza na uokolewe umilele kwa ukamilifu wake wa uwezo.